## MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA MWEZI SEPTEMBA, 2025 NA MWELEKEO KWA MWEZI OKTOBA, 2025.

**Dondoo za tathmini ya Septemba, 2025 na mwelekeo wa Oktoba, 2025:**

Taarifa hii inatoa muhtasari wa mifumo ya hali ya hewa pamoja na mwenendo wa hali ya hewa kwa mwezi Septemba, 2025 na kutoa mwelekeo wa hali ya hewa kwa mwezi Oktoba, 2025 nchini.

i. Katika kipindi cha mwezi Septemba, 2025 hali ya ukavu pamoja na vipindi vya baridi hususan katika nyakati za usiku vilijitokeza katika maeneo machache. Hata hivyo, vipindi vichache vya mvua vilijitokeza katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa pwani, nyanda za juu kaskazini mashariki na ukanda wa ziwa Victoria.

ii. Katika kipindi cha mwezi Oktoba 2025, mvua za Vuli zinatarajiwa kuanza katika maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Aidha, mvua za chini ya wastani hadi wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi.

iii. Katika kipindi cha Oktoba, 2025, ongezeko kidogo la joto linatarajiwa katika baadhi ya maeneo.

## 1.0 MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI SEPTEMBA, 2025.

Katika kipindi cha mwezi Septemba, 2025 hali ya ukavu iliendelea kujitokeza katika maeneo mengi ya nchi, pamoja na vipindi vya baridi kiasi hususan nyakati za usiku katika maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi. Kiwango cha chini kabisa cha joto kiliripotiwa kua nyuzi joto 5.4 °C katika kituo cha Uyole (Mbeya) mnamo tarehe 6 Septemba. Aidha, viwango vya joto la juu viliongezeka kidogo katika maeneo mengi ya nchi. Mnamo tarehe 29 Septemba, 2025 kituo cha Mpanda kilichopo mkoa wa Katavi kiliripoti kiwango cha juu zaidi cha nyuzi joto 36.6 °C. Kwa upande mwingine, vipindi vichache vya mvua vilijitokeza katika maeneo ya ukanda wa pwani na nyanda za juu kaskazini mashariki. Aidha kwa

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

ukanda wa ziwa Victoria vipindi vya mvua iliyoambatana na ngurumo za radi vilijitokeza. Kiwango cha juu zaidi cha mvua cha milimita 44.2 kilipimwa katika kituo cha hali ya hewa Bukoba (mkoa wa Kagera) mnamo tarehe 15 Septemba, 2025. Aidha, vipindi vifupi vya upepo mkali unaofikia kasi ya km 40 hadi 50 kwa saa vilijitokeza katika baadhi ya maeneo nchini, hususan ukanda wa pwani na maziwa makuu.

## 2.0 MWELEKEO KWA MWEZI OKTOBA, 2025

### 2.1 MIFUMO YA HALI YA HEWA

Katika kipindi cha mwezi Oktoba, 2025 joto la bahari katika eneo la kati la kitropiki ya bahari ya Pasifiki linatarajiwa kuwa la chini ya wastani, ikiashiria uwepo wa hali ya *La Niña* hafifu. Aidha, joto la bahari katika eneo la magharibi mwa Bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa chini ya wastani, huku joto la juu ya wastani likitarajiwa katika eneo la mashariki mwa bahari ya Hindi. Hali hii inatarajiwa kuwa na mchango hafifu wa kusababisha upepo wenye unyevu kuvuma kuelekea ukanda wa pwani pamoja na maeneo jirani ya pwani. Katika eneo la karibu na pwani ya Angola, hali ya joto la bahari ya chini ya wastani inatarajiwa na hivyo kuwa na mchango kiasi katika kusababisha upepo wenye unyevu kuvuma kutoka misitu ya Congo kuelekea maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria na magharibi mwa nchi. Hata hivyo, joto la bahari la juu ya wastani katika ncha ya kusini mwa Afrika linatarajiwa kuendelea na hivyo kupunguza uwepo wa hewa yenye ubaridi kutoka kusini na kusababisha ongezeko la joto katika baadhi ya maeneo nchini.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

## 2.2 HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI OKTOBA, 2025

Katika kipindi cha mwezi Oktoba 2025, mvua za msimu wa Vuli zinatarajiwa kuanza katika maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Aidha, mvua za chini ya wastani hadi wastani pamoja na mtawanyiko hafifu zinatarajiwa katika maeneo mengi. Kwa upande mwingine, hali ya joto kiasi hadi joto kali inatarajiwa hususan katika maeneo yanayotarajiwa kupata vipindi vichache vya mvua. Vipindi vya upepo mkali vinatarajiwa kujitokeza hususan katika maeneo ya ukanda wa pwani na maziwa makuu. Ufuatao ni mwelekeo wa hali ya hewa nchini;

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba):**

Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika wiki ya tatu kwa baadhi ya maeneo haya.

**Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):**

Vipindi vifupi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika wiki ya nne.

**Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu):**

Vipindi vya mvua inayoambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa wiki katika wiki ya nne ya mwezi.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):**

Vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo katika kipindi cha mwezi Oktoba,2025. Ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa kuelekea mwishoni mwa mwezi.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):**

Kiujumla, hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi, Aidha, vipindi vichache vya mvua vinaweza kujitokeza katika maeneo machache.

**Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro):**

Hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi. Aidha, vipindi vichache vya mvua na hali ya baridi kiasi inatarajiwa katika maeneo ya miinuko.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):**

Vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache ya mwambao wa pwani. Ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa kujitokeza kati ya wiki ya tatu na ya nne ya mwezi.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma):**

Hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi. Aidha, vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika maeneo ya miinuko.

### 2.3 MATARAJIO KWA MWEZI NOVEMBA, 2025

Katika kipindi cha mwezi Novemba, 2025 vipindi vya mvua vinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo nchini. Ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika baadhi ya

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

maeneo. Joto la wastani hadi juu ya wastani linatarajiwa kuendelea kujitokeza kwa baadhi ya maeneo nchini.

**2.4 USHAURI**

Mvua za Vuli, 2025 zinatarajiwa kuanza mwezi Oktoba, 2025 katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Vipindi vya mvua kubwa vinatarajiwa kujitokeza, hivyo wananchi wanaoishi katika maeneo yanayoathiriwa na mafuriko wanashauriwa kuendelea kuchukua hatua stahiki ili kupunguza athari zitakazojitokeza.

*Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, Mamlaka za Wanyamapori, Mamlaka za Maji na Afya waendelee kutafuta, kupata na kufuata ushauri wa wataalamu katika sekta husika.*

Imetolewa tarehe 01 Oktoba, 2025 na:

**MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA.**

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

*727B - 02/2023*